



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Disemba 11, 2020

Wapenzi Familia wa Lowell Public Schools,

Ninatarajia kwamba barua hili litapata kila mtu akiwa salama na mwenye afya katika muda huu mgumu. Tangu Oktoba tarehe 19, asilimia 97% ya wanafunzi wetu wamekuwa wakishiriki katika mafunzo ya mbali kwa sababu ya viwango vinavyozidi vya COVID-19 hapa Lowell. Wakati huo huo asilimia ndogo ya wanafunzi wetu walio katika madarasa maalum yaliyo tofauti zaidi na madarasa ya kawaida wameendelea kuwa na chaguo la kuhudhuria masomo darasani, tangu siku ya kwanza ya shule. Katika mgogoro huu wa kiafya usiyoweza kutabirika, tumepatia kipaumbele kuwawezesha wanafunzi wetu walio dhaifu zaidi kuwa shuleni kwa sababu ya mahitaji yao yaliyo maalum zaidi na kwa sababu ya huduma na mafunzo husika wanayopokea kila siku.

Tunaendelea kuamini kiwango cha usalama katika shule yetu na itifaki thabiti za wilaya zinazotekelezwa, lakini usambazaji wa jamii yote ya COVID-19 – ambayo imezidi kuongezeka na kufikia zaidi ya matukio 100 katika watu 100,000 wa Lowell wiki hii iliyopita – itaendelea kuwa na athari zaidi kwa upatikanaji wa wafanyikazi na uwezo wa upatikanaji wa wafanyikazi mbadala kwa sababu ya kuwemo hatari wa virusi na karantini. Katika kasi ya sasa, kiwango cha usambazaji wa kijamii wa COVID-19 kwa uhakika utafika kiwango ambacho utavuruga uendeleu wa mpango wa kuhudhuria shuleni katika siku zijazo huku tukilazimika kuweka karantini madarasa na mashule binafsi. Kwa hivyo, ili kuwapatia familia arifa ya kutosheleza iwezekanavyo na kuondoa uwezo wa kubadilisha mpango kwa mpango wa mafunzo ya mbali mara moja (ambayo italetwa na itifaki yetu ya karantini), **programu zote za masomo maalum yaliyo tofauti zaidi na masomo ya kawaida na yanayotekelezwa shuleni sasa zitabadilishwa kwa mafunzo ya mbali katika wiki ya nusu kabla ya likizo ya majira ya kipupwe, ikiwamo:**

Jumatatu, Disemba 21

Jumane, Disemba 22

Jumatano, Disemba 23

Wanafunzi hawa wataendelea kuhudhuria shule kwa wiki ijayo ya Disemba 14-18, na tunapanga kuwarejesha wanafunzi hawa kwa mafunzo ya kuhudhuria ibinafsi haraka iwezekanavyo baada ya likizo ya majira ya kipupwe, huku siku ya kwanza shuleni ikipangiwa kuwa Jumatatu, Januari tarehe 4.

Tunafahamu athari ambazo maamuzi haya magumu zinazo kwa wanafunzi na familia, kwa hivyo barua hili limekusudiwa kupatia arifa ya mapema iwezekanavyo kuwawezesha familia kupangia kwa siku hizi (3) za mafunzo ya mbali yaliyoorodheshwa hapa juu.

Wanafunzi waliobaki watahudhuria mafunzo ya mbali shuleni, tutaendelea na mpango wetu wa sasa wa mafunzo ya mbali hadi hali ibadilike. Tunapanga kuwapatia familia taarifa hadi likizo ya majira ya kipupwe.

Asante sana tena kwa utendakazi wako unaoendelea na uwezo wako wa unyambuliko tunapojitahidi kulinda wanafunzo, familia na wafanyikazi wetu katika muda huu mgumu na usiyo na uhakika.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Msimamizi Mkuu wa Mashule